# Tanzania, Burundi zaitwa kujiunga viza ya pamoja kwa watalii



Sokwe ni moja ya vivutio vingi vya kitalii vilivyopo katika mbuga za wanyama katika nchi za Afrika Mashariki. **Picha na Maktaba**

**Alawi Masare**, Mwananchi

Akiwa na viza ya pamoja ya utalii kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki(EAC), mtalii anaweza kutembelea nchi yoyote katika jumuia hii lakini siyo Tanzania wala Burundi.

Nchi hizo mbili zilikataa kujiunga na mfumo huu tangu ulipozinduliwa mwanzoni mwa mwaka 2014 na nchi tatu za Uganda, Kenya na Rwanda ambazo ziliamua kuendelea na mpango huo.

Viza ya pamoja ya utalii ilianzishwa ili kurahisisha upatikanaji wake kwa watalii, hivyo kuifanya Jumuia kama nchi moja na pia kupunguza gharama za uingiaji.

Kwa sasa, viza hiyo inayotumika kwa siku 90, inagharimu dola za Marekani 100 badala ya 150 zilizokuwa zikitozwa na kila nchi na watalii wanaweza kuiomba katika ofisa yoyote ya uhamiaji ya Uganda, Kenya na Rwanda au kwenye mtandao wa internet. Burundi na Tanzania bado hazijajiunga na mpango huo.

Hata hivyo, shinikizo linajitokeza kutoka taasisi za sekta ya umma na binafsi, ni kwa Tanzania na Burundi kujiunga na mpango huo ili iwe rahisi kuitangaza Afrika Mashariki kama kituo kimoja cha utalii. Ukanda wa Afrika Mashariki una vivutio mbalimbali vya asili ambayo baadhi yao vipo katika orodha ya maajabu ya Afrika.

Baadhi ya wadau wa sekta ya utalii wanasema kwamba Tanzania na Burundi zisidhani kwamba "zinaishi kwa kutengwa" na kwamba nchi hizo mbili zinatakiwa kujiunga, ili kupunguza gharama watalii kuingia na hivyo kuvutia wageni wengi zaidi Afrika Mashariki.

Utaratibu huu wa viza ya pamoja unalenga kurahisishia watalii kuingia katika nchi zote na hivyo kutengeneza mazingira ya wao kutumia fedha wakati wanapozuru vivutio mbalimbali katika nchi yoyote mwanachama.

"Ningependa kuwaambia kaka na dada zetu kutoka nchini Tanzania na Burundi kwamba tuko katika mkoa mmoja na wanapaswa kujiunga ili tufanye jitihada za pamoja kutangaza vivutio vyetu kama kituo kimoja cha utalii," anasema Stephen Asiimwe, Ofisa Mtendaji mkuu wa Bodi ya Utalii Uganda wakati akitangaza kuanza kwa maonyesho ya pili ya utalii wa Uganda hivi karibuni.

Naye mwenyekiti wa Jukwaa la Utalii Afrika Mashariki (EATP),Manzi Kayihura, anasema:" Wanapaswa kutambua kwamba sisi hatushindani bali tunashirikiana katika kuitangaza jumuia yetu."

EATP imeanzishwa kwa misingi ya kukuza utalii wa ndani na baina ya nchi, utetezi, masoko, pamoja na kugawana taarifa za kiutafiti.

Uganda ambayo inalenga kufikia watalii milioni 1.5 ndani ya miaka mitano ijayo, ilikuwa mwenyeji wa wadau wa huduma za kitalii wapatao 40 kutoka duniani kote, ambao walitembezwa katika vivutio mbalimbali nchini humo.

Uganda iliwaonyesha vivutio vyake vya utamaduni kama vile jamii ya Batwa wanaopatikana eneo la Mgahinga na kituo cha Ndere ambacho huburudisha kwa nyimbo na michezo yenye elimu tele.

Safari hiyo pia ilihusisha pia utafutaji sokwe, wanyama wanaofanana na binadamu ambao hupatikana Uganda na Rwanda kwa nchi za Afrika Mashariki.

Wadau hao walijumuisha waandishi wa habari, bodi za utalii na watoa huma za utalii kutoka ndani na nje ya Afrika.

Mkurugenzi wa Sigo Adventures and Tours, kutoka Lusaka, Zambia Walter Joe Syakalonga, anadhani nchi zote za Afrika Mashariki zina uzoefu tofauti.

"Nimesikia watu wakijaribu kulinganisha kuonekana kama mashindano, lakini nadhani itakuwa si vizuri kushindana ndani ya kanda. Pamoja na ukweli kwamba baadhi ya vivutio vinapatikana katika nchi zote mbili, uzoefu ni tofauti. Uganda na Rwanda wana sokwe lakini ladha ni tofauti,anasema.

### Sekta binafsi Tanzania

Wakati Serikali ya Tanzania bado inaendelea na msimamo wake wa kubaki nje ya mfumo wa viza ya pamoja, sekta binafsi nchini haioni sababu ya kuwa na wasiwasi kuhusu hilo.

Sekta binafsi inaitaka Serikali kufanya tathmini au kufanya utafiti ili kujiridhisha jinsi mfumo huo unaweza kuongeza au kupunguza mapato ya utalii na kufanya uamuzi lakini ina matumaini kwamba watalii wataongezeka.

"Tayari Tanzania ni ghali katika viwanja vya ndege na kufanya karibu asilimia 70 ya watalii wake kuja kupitia Kenya. Viza ghali ni gharama nyingine ambayo nadhani itakatisha tamaa wasafiri," anasema Mkurugenzi mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF),Godfrey Simbeye.

Anaongeza:"Tanzania ina vivutio vingi kiasi kwamba kila mgeni ajaye katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki angependa kuviona kabla ya kuondoka. Hivyo, hata kama mapato ya viza yatapungua, itafidiwa na ongezeko la watalii ambao watatumia pesa katika hoteli zetu.''

### Mgawanyo ulivyo

Kwa ushirikiano unaoendelea Kati ya nchi tatu zinazoshirikiana mpaka sasa, mgawanyo wa mapato umetengenezewa utaratibu wake. Nchi yoyote itakayopokea mgeni inapata asilimia 40 ya kiasi chote kitakachopatikana.

miongoni mwa vikwazo vilivyoichelewesha Tanzania kujiunga kwenye makubaliano hayo, inaelezwa kuwa ni kuupitia utaratibu huo na kuona nanmna itavyoongeza idadi ya wageni inaopokea kila mwaka kwa kuzingatia sekta yake ya anga inayosuasua ikilinganishwa na ile ya Kenya.

Miongoni mwa mataifa yanayounda EAC, Kenya ina usafiri makini wa anga ambao ndiyo kichocheo kikubwa cha kufanikisha ukuaji wa utalii duniani. Shirika la Ndege la Tanzania ni kama halipo kwa sasa baada ya kutokuwa na ndege hata moja inayofanya safari.

**SAUTI ZA WANANCHI**

**Marick Manyamba:**

**Ili kujenga mazingira mazuri ya biashara, Serikali inatakiwa kuandaa kongamamo kati ya wafanyabiashara wadogo na wakubwa ili kujenga urafiki kati yao, kwa lengo la kupunguza kodi ambazo sio za lazima kwa biashara ndogo ndio wananchi wengi wa kipato cha chini waweze kumudu na kupata faida ambayo itawawezesha kulipa kodi kwa wakati.**

**Javan Adika:**

**Ili kuboresha mazingira ya biashara nchini, kuwa na mahali pamoja ambapo leseni zote zinalipiwa na kutolewa, pamoja na kodi na tozo zote. Leseni zote zipatikane ndani ya muda usiozidi siku tatu baada ya mwombaji kutimiza masharti yote. Wafanyabiashara wasitozwe kodi hadi wafanye biashara kwa angalau mwaka mmoja**

UKURASA HUU UMEDHAMINIWA NA
BEST-Dialogue
Doing business, let's make it easy - and fair
Kufanya biashara kwa haki - bila vikwazo